**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MUU - TAMISEMI**
**MKOA WA SINGIDA HALMASHAURI YA**
**WILAYA YA MKALAMA SHULE YA**
**SEKONDARI IGUGUNO**
**S.L.P 55**
**SINGIDA**

**MKUU WA SHULE 0713-986-798/0756-986-798**
**MAKAMU MKUU WA SHULE 0769-581-662/0622-072-866**
**MUHASIBU WA SHULE 0763-913-455/0620-640-297**

MZAZI WA..............................................................
S.L.P: .........................................................................

**YAH: <u>KUJIUNGA NA KIDATO CHA………..MWAKA ………………</u>**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao................................................................... Amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano hapa Iguguno Sekondari katika Tahasusi ya........................Ni matumaini yetu kuwa wewe Mzazi/Mlezi utashirikiana na Uongozi wa Shule katika malezi ili mwanao aweze kuitumia nafasi hii adhimu kwa manufaa yake na Taifa kwa ujumla. Shule itafunguliwa na masomo kuanza pindi serikali itakapotoa maelekezo ya kufungua shule (**NI VYEMA KUFUATILIA TAARIFA MBALIMBALI KUTOKA SERIKALINI).** Mzazi/Mlezi ni wajibu wako kulipa Michango yote ya shule. Ieleweke kuwa siyo jukumu la Mkuu wa shule kusamehe kulipa Michango yote ya shule bali wewe Mzazi/Mlezi ufanye mipango ya kupata na kulipa michango hiyo.

**NB**: Mwanao hataandikishwa shuleni bila kukabidhi ofisini nakala halisi na nakala ya vivuli vya vyeti vilivyoagizwa katika ukurasa wa 08 na fomu zote za usajili zilizoambatanishwa katika barua hii ya kujiunga zikiwa zimejazwa kikamilifu viambatisho A, B na C ukurasa wa 9,10,11 na 12

**MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUWEPO SHULENI BILA KUSAJILIWA.**

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Iguguno ipo Mkoa wa Singida Wilaya ya Mkalama, kilometa 35 toka Singida Mjini. Usafiri wa kufika Iguguno kutoka Singida Mjini hadi stendi ya mabasi Iguguno ni wa Daladala, Kwa kawaida bei ya Daladala ni Tsh. 3,000/= na kutoka Singida Mjini hadi Iguguno stendi. Kutoka Iguguno stendi hadi shuleni atatumia usafiri wa Bodaboda au Bajaji nauli yake ni Tsh 2000/=

**NB:**Kwa wanaotoka mikoa ya Kanda ya ziwa mfano Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kagera, Geita Mara na Simiyu wanatakiwa kushukia stendi ya Iguguno.

**A. MICHANGO YA SHULE**

Fedha zote za michango zilipiwe benki kwa kuzingatia maelekezo ya namna ya kulipa yaliyotolewa hapo chini. Hati ya malipo **(BPS) iandikwe majina ya mwanafunzi na kidato**. **(Mfano: Hamisi Juma James F.5 HGL) usiandike jina la mlipaji (mzazi /mlezi).** Mwanafunzi alete shuleni **"Original Bank Pay in Slip" (BPS)** moja ya michango uliyolipia. BPS hiyo amkabidhi mhasibu na atapewa stakabadhi. Hatupokei fedha Taslimu. **NB:** HAKIKISHA KUWA MWANAO ANALIPA MICHANGO YOTE ANAPORIPOTI SHULENI**.**

**NAMNA YA KULIPA ADA NA MICHANGO MINGINE**

Michango yote ya shule ilipwe kupitia Bank ya NMB A/C No. **50601100154** Jina la Akaunti ni ***IGUGUNO SECONDARY SCHOOL RECURRENT.***

Tafadhali zingatia utaratibu huu bila kukosea na Original Bank Pay in Slip aje nayo shuleni. **NB:** USIWEKE FEDHA ZA MATUMIZI YAKO KWENYE AKAUNTI HIYO**.** Andika nyuma mchanganuo wa michango uliyolipa pamoja na majina yako kamili

**B. MCHANGANUO WA MALIPO**

| S/N | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango Wa Uendeshaji Wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## C. SARE ZA SHULE

### (a) Wavulana

- **Sare ya darasani**
  - i. Sare ya shule hii ni Suruali mbili rangi "Dark Blue" zenye mapana ya inchi 16.
  - ii. Mkanda wa ngozi mweusi wenye upana wa kawaida (usiwe na chater yoyote) wavulana tu.
  - iii. Sweta la shule ni rangi ya "Dark Blue" kola ya V,
  - iv. Mashati mawili meupe mikono mirefu (Tomato)
  - v. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kamba.
  - vi. Soksi jozi mbili au zaidi za rangi nyeusi zisizo na mistari
  - vii. CHF na huduma ya kwanza....................................**Tshs. 50,400** aje Na fedha mkononi kila mwaka wa masomo (Ni agizo la serikali kila mwanafunzi kuwa Na Bima ya Taifa NHIF)

- **Sare za kushindia wavulana**,
  - i. Suruali 02 za rangi ya kaki, shona mwenyewe (ishonwe kwa vipimo vifuatavyo; mifuko miwili pembeni kwa mbele, mfuko mmoja nyuma upande wa kulia, isiwe box pocket, marinda mawili kila upande kwa mbele. Suruali iwe saizi ya kawaida isiyoshika, kubana mwili (kimodo) inchi 16 upana usawa wa kuanzia soli ya kiatu, yenye mkunjo kwa chini (turn up) na isiwe na urembo wowote.
  - ii. T-shirt 2 za kushindia r angi ya golden yellow Na aweke nembo iliyoko juu ya fomu hii

### (b) Wasichana

- **Sare ya darasani**:
  - (i) Sketi 2 za "Dark Blue"
  - (ii) Kwa waislamu watashona nusu kanzu nyeupe mbili ambazo ni ndefu ikiambatana na hijabu nyeupe mbili ndefu zinazofunika tumbo.
  - (iii) Mashati mawili meupe (Tomato) ya mikono mirefu na yenye mfuko mmoja kwa wanafunzi wasio waislamu.
  - (iv) Viatu vya ngozi vyeusi **vyenye kamba** jozi mbili, visiwe na visigino virefu "Safari boots na viatu vya wazi" **(simple haviruhusiwi).**
  - (v) Soksi jozi mbili (Stockings).
  - (vi) CHF na huduma ya kwanza ....................................**Tshs. 50,400** kila mwaka wa masomo aje Na fedha mkononi (Ni agizo la serikali Kila mwanafunzi kuwa Na Bima ya Taifa ya NHIF)

- **Sare ya kushindia wasichana** (Shamba dress),
  - (vii) Sketi 2 ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu za rangi ya kaki ashone mwenyewe kwa vipimo vifuaavyo; rinda tatu upande wa kushoto na kulia lazima iwe ndefu kuanzia kwenye kifundo cha mguu. (Ni lazima)
  - (viii) T-shirt 2 Rangi ya golden yellow Na aweke nembo iliyoko juu ya fomu
  - (ix) Juba la rangi ya njano (kitambaa cha Tetron nzito) (iii) Kanga pair moja.

**NB**: Ni marufuku kuja na juba yenye urembo.

- Nguo **za michezo kwa wavulana na wasichana.**

i. Sare za michezo **(anunue au aje na fedha mkononi Kwa ajili ya Tracksuit full na t-shirt zinapatikana shuleni kwa Tsh 36,000**
ii. Bukta ya rangi ya kijani.
iii. Raba kwa ajili ya michezo rangi yoyote.

NB;**Nguo za nyumbani haziruhusiwi (Atakayekuja na nguo isiyo sare ya shule atarudishwa nyumbani).**

**USAFI BINAFSI WA MWILI**

- Nywele fupi za kuchana kwa kitana kidogo, kunyoa kiduku/panki ni marufuku
- Ndefu na mustachi havitakiwi
- Kuoga kila siku ni lazima
- Huruhusiwi kufuga kucha na kupaka rangi kwenye kucha na mdomo
- Kuvaa kofia, bangili, herein, kipini, kidani, (mkufu) na kikuku haviruhusiwi shuleni

**D. VIFAA VYA SHULE**

(i) Bunda 02 za karatasi za "Photocopy A4 kwa wanafunzi wote (mbili kwa kila muhula wa masomo)
(ii) Ufagio wa chelewa moja ataleta kila mwanzo wa mwaka wa masomo (wote)
(iii) Soft broom moja
(iv) Skwiza (mopa) moja
(v) Ndoo moja lita 10 wote (kwa ajili ya matumizi ya shule)
(vi) Jembe moja lenye mpini **HGK**
(vii) Brash ya kusafishia chooni (TOILET BRUSH)
(viii) Shoka moja lenye mpini **HGE**
(ix) Panga moja **HGL**

**E. MAHITAJI YAKE BINAFSI**

(i) Fedha za matumizi binafsi pamoja na nauli. Ni vizuri akafungua akaunti ili kuifadhi fedha hizo shule inaweza kusaidia zoezi la kufungua akaunti benki akifika shuleni mpatie kiasi cha Tsh10,000/= kwa ajili ya kufungua akaunti.
(ii) Taulo,
(iii) Ndala, Mswaki, Dawa ya meno ipo duka la shule, Sabuni, mafuta ya kupaka,
(iv) **Ndoo moja ya kuogea** na chombo cha kutunzia maji ya kunywa (kidumu cha lita (5) tano) Vyombo vya kulia chakula.
(v) Madaftari makubwa 8 (counter Book Quire 3).
(vi) "Scientific Calculator" na "Mathematical set" kwa wanafunzi wanaosoma Hisabati, Sayansi na Geografia na kutokana na uhaba wa vitabu Mzazi mnunulie vitabu mwanao orodha imeambatanishwa.
(vii) Faili moja kwa kila somo kwa ajili ya kutunzia vitini (handouts) mbalimbali na karatasi zake za majaribio na mitihani ya muhula.
(viii) Aje na Godoro moja lenye futi **2½** kwa 6 inch 4, shuka 2 (anunue au aje Na fedha kununu Shuka Aina ya Polytex light blue 01 na pink 01, blanketi moja na chandarua cha ukubwa wa futi3 kwa 6, cha duara, mto na foronya ya rangi ya pink/bluu.

***Vifaa vyote vilivyoagizwa vitakaguliwa katika ofisi ya usajili kabla ya mwanafunzi kusajiliwa**

**MAWASILIANO:**

i. Mzazi/Mlezi utatumia namba za simu zifuatazo kwa mawasiliano na mwanao **0758 555 039** au 068646040 **PATRON (mwalimu mlezi wa kiume kwa wanafunzi wa kiume tu)**
ii. **0682413050 MATRON (mwalimu mlezi wa kike kwa wanafunzi wa kike tu)**

**NB:** Mzazi /mlezi tumia namba hizo hapo juu tu kumtumia mwanao fedha za matumizi akiwa shuleni pamoja na nauli wakati wa likizo.Shule haitahusika na usumbufu wowote endapo utatumia namba tofauti na zilizotajwa hapo juu.

**F. MATIBABU:**

Matibabu yanafanywa kwenye Zahanati ya Iguguno kwa kutumia mpango wa tiba kwa kadi **(CHF)** iliyoboreshwa kwa shilingi **50,400.** Kwa kuwa shule haina usafiri, mwanao anatakiwa kulipa shilingi 5,000 kwa mwaka kwa ajili ya huduma ya usafiri pindi anapo umwa Wanafunzi wenye kadi za Bima ya afya hawana haja ya kulipa mchango wa matibabu kwa kuwa wanaweza kutumia kadi zao. Ila watalipa Tsh. 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza (usafiri) kwa mwaka.

**G. MIPAKA YA SHULE.**

Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali cha Mkuu wa Shule na lazima mwanafunzi avae sare za shule akitoka nje na awe na kibali kilichosainiwa na Mkuu wa shule.

**H. SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUTEMBELEA** Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo wakati wowote hata anapokuwa likizo

a) Vilabu vyote vya pombe (Bar na night clubs)

b) Majumba ya starehe (Cinema halls, Disko halls n.k)

c)Nyumba za watumishi bila ruhusa.

**I. WAKATI WA LIKIZO: Mwanafunzi haruhusiwi kubaki shuleni wakati wa likizo**.Hivyo Mzazi/Mlezi hakikisha unamtumia mwanao fedha za kutosha kwa ajili ya nauli wakati shule inapokaribia kufungwa kwa kutumia namba za simu za Matron au Patron AU kwenye akaunti Binfsi ya mwanafunzi.

**(J) SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria Ya Elimu Na.25 Ya Mwaka 1978** pamoja na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na itakayotolewa na Wizara zenye dhamana ya Elimu nchini. Anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo na yatafafanuliwa mara kwa mara baada ya kuripoti shuleni:

i. Heshima kwa viongozi, Wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule na kukamilisha kazi ni muhimu. iii. Kutimiza kwa ukamilifu maandalio ya jioni na usipige kelele uwapo darasani.

iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopewa.

iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote.

v. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule ni lazima kwa kila mwanafunzi. vii. Kuvaa sare za shule wakati wote wa shule na anapotoka nje ya eneo la shule. viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

vi. Mwanafunzi hataruhusiwa kumiliki simu ya mkononi, kamera, redio wala kuongea na mgeni asiyeruhusiwa shuleni

vii. Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa nguo zisizo sare za shule wakati wote awapo hapa.

viii. Mwanafunzi haruhusiwi kusomea nje ya madarasa, bwenini au bwaloni au darasa lisilo lake.

ix. Kutumia lugha ya heshima kwa walimu na watu wengine hata wao kwa wao.

x. Ni ofisi ya shule tu itakayopokea taarifa za dharura za mwanafunzi kama vile msiba, ugonjwa nk.

xi. Hairuhusiwi wanafunzi kuandikiana barua

xii. Mwanafunzi aingiapo ofisini lazima apige/agonge hodi kabla ya kuingia

xiii. Mwanafunzi awapo safarini lazima avae sare za shule.

xiv. Hairuhusiwi kwenda kwenye nyumba za watumishi bila ruhusa maalumu.

xv. Upotevu/uharibifu wowote bwenini/darasani utalipwa na wakazi husika.

xvi. Huruhusiwi kuwa bwenini wakati wa masomo au kuwa darasani wakati na kulala. (Ni lazima kufuata ratiba ya kila siku ya shule)

xvii. Ni marufuku kutoka shuleni bila ruhusa ya maandishi.

**K. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI**

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga
3. Uvutaji bangi
4. Ulevi wa pombe au madawa ya kulevya kwa mfano cocaine, mirungi, kuberi n.k
5. Kutofika sehemu ya parade/Roll call, kulala nje ya shule (utoro)
6. Kupigana au Kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
8. Kudharau bendera ya Taifa, viongozi, walimu na vitu vya kitaifa.
9. Kuoa/Kuolewa, kupata/kutoa mimba, kusababisha mimba nje au ndani ya shule.
10. Ubaguzi wa aina yoyote (dini,kabila, jinsi,nk)
11. Kupatikana na simu ya mkononi shuleni.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani, mali na usalama wa shule na watu kwa ujumla.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Utoro wa zaidi ya siku 90 bila ruhusa ya maandishi**.**
15. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi**.**
16. Kuonywa mara 3 bila kubadilika.
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kuua (kwa kutumia sumu, kamba, dawa nk).

**L. MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA**

i. Unapaswa kujaza Viambata vyote vilivyo amatanishwa na fomu hii Viambata hivyo ni kiambata **A, B** na **C**
ii. Mwanafunzi anaporipoti shuleni awe amevaa shamba dress.
iii. Aje na passport size za ndugu wa tatu watakaotambuliwa na shule.

**M. VITABU**

Mzazi unaweza ukamnunulia mwanao vitabu vifuatavyo kulingana na tahasusi aliyopangiwa;

| NA. | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| 1. | GEOGRAPHY | i. Human and Economic Geography Advanced level.- **D.T Msabila.**<br>ii. Practical Geography Advanced Level (Map Reading, Photography Interpretation Field Research, Statistics & Introductory to Survey).<br>iii. Geography an Intergrated Approach – **David Waugh**<br>iv. Physical Geography for Secondary Schools - **D.T Msabila**<br>v. Physical Geography of Africa with Diagrams - **Burnett** |
| 2. | HISTORY | i. History for Secondary Schools Form Five – **T.I.E (2016)**<br>ii. History for Secondary Schools Form Six – **T.I.E (2016)**<br>iii. Contemporary Historical Events Advanced Level History One **Tumaini, S.C.K (2010).**<br>iv. Essentials in Advanced Level History Paper 2, **Yassin, S.**<br>v. History of Modern Europe in the 19th Century – **P. Cock** |
| 3. | GENERAL STUDIES | i. General Studies for Advanced Level Certificate Form Five – **Richard R. F Mbalase.**<br>ii. General Studies, Supplimentary Book For Advanced Level and Colleges, **- Konrad Adenaker Stiftung, 2nd** Edition |
| 4. | ECONOMICS | **i. PRINCIPLE OF ECONOMICS –M.L JHINGAN**<br>ii. Principles of Economics – **N. A Saleemi.**<br>iii. A Text Book of Economics – **DWIVEDI, D.N** 7th Edition.<br>iv. Basic Economics – **Tayebwa B. Mugisha, 5th Edition (2011).**<br>i. |
| 5. | BASIC APPLIED MATHEMATICS | i. Basic Applied Mathematics – **Kiza and Septine I Sillem.**<br>ii. Advanced Mathematics – **Shayo**<br>iii. Advanced Mathematics Book 1 & 2 – **Backhouse**<br>iv. Advanced Mathematics - **Chand's 1 & 2** |
| 6. | KISWAHILI | i. Kiswahili Kidato cha Tano – **T.I.E**<br>ii. Kiswahili Kidato cha Sita – **T.I.E**<br>iii. Nadharia ya Fasihi kidato cha Tano na Sita **– Nyambari Nyangwine**<br>iv. Nadharia ya Lugha Kidato cha Tano na Sita – **T.I.E**<br><br>❖ **RIWAYA**<br>i. Usiku Utakapokwisha<br>ii. Vuta N'kuvute<br>iii. Mfadhili<br>iv. Kufikirika<br><br>❖ **TAMTHILIYA**<br>i. Morani<br>ii. Kivuli Kinachoishi<br>iii. Kwenye Ukingo wa Thim<br>iv. Nguzo Mama |

| | | |
|---|---|---|
| | | ❖ **USHAIRI**<br>i. Kimbunga<br>ii. Fungate ya Uhuru<br>iii. Mapenzi Bora |
| 7. | ENGLISH LANGUAGE | ❖ **ENGLISH LANGUAGE I**<br>i. Advanced English Language I- Shadrack Ndambo<br>ii. Advanced level English Language i- Nicholous Asheri<br>iii.<br>❖ **ENGLISH LANGUAGE II**<br>Advanced level Literature Analysis<br>• **NOVEL**<br>i. A man of the people<br>ii. The Beautiful ones are not yet born<br>iii. His excellent the head of state<br>• **PLAYS**<br>i. An enemy of the people<br>ii. Betrayal in the city<br>iii. I will marry when I want<br>**iv.** Lwanda magere<br>• **POETRY**<br>i. Selected poems<br>ii. The wonderful surgeon |

**MWISHO**

Shule inathamini umoja, amani na juhudi katika masomo, tabia na kazi za nje. Nidhamu safi ni msingi wa mafanikio ya kila binadamu hivyo, kila atakaye kubali kujiunga na shule hii atatakiwa kuzingatia haya. Sheria za shule zimeambatanishwa zisome kwa makini na uwe tayari kuzifuata.Aidha uelewe kuwa sheria ni mwongozo wa kukuelewesha mambo ambayo hayatakiwi kufanywa. Muhimu kwako ni kutumia akili na busara na si rahisi kutunga sheria za kila kosa linaloweza kufanywa na mwanafunzi hivyo zingatia **NIDHAMU NA BIDII** kwa kila jambo itakupa uwezo wa kujenga msingi imara na maendeleo yako,ya shule na taifa kwa ujumla. Nakutakia heri na mafanikio ukiwa katika Shule hii na Ni matumaini yangu daima utatii sheria, taratibu na kanuni za Shule ili uje uvune kile kilicho kuleta shuleni.

**ELIMU NA UJUZI**

**HONGERA NA KARIBU SANA IGUGUNO SEKONDARY**

THE HEADMISTRESS
IGUGUNO SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 55-SINGIDA

**PHILLY E. NYAWADE**

**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATANISHO "A"**

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI IGUGUNO
FOMU YA MAELEZO BINAFSI (PERSONAL PARTICULARS)
KWA AJILI YA USAJILI (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

1. Jina kamili la mwanafunzi kama alivyojiandisha kwenye mtihani wa kidato cha nne
------------------------------------------------------------------------------------------------------------

2. Jina kamili la baba Mzazi/Mlezi---------------------------------------------------------------------------
i. Anwani ya Baba /Mlezi-------------------------------------------------------------------------------------------
ii. Nambari ya simu ya Baba/Mlezi kazini-------------------------------------------------------------------
Nyumbani------------------------------------------------------------------------------------------------------------
iii. Mtaa/Kijiji-------------------------Kata------------------------Tarafa------------------------Wilaya--
-----------------------------------------------------anakotoka

3. Jina kamili la Mama Mzazi/Mlezi-----------------------------------------------------------------------
i. Anwani ya Mama /Mlezi--------------------------------------------------------------------------------------
ii. Nambari ya simu ya Mama/Mlezi -----------------------------------------------------------------
Nyumbani------------------------------------------------------------------------------------------------------------
iii. Mtaa/Kijiji-------------------------Kata------------------------Tarafa------------------------Wilaya-
--------------------------------------------------------anakotoka

4. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi-----------------------------------------------------------------------------
5. Mahali alipozaliwa---------------------------------------Mkoa------------------------------------------
Wilaya--------------------------------------------------------Kijiji/Mtaa-------------------------------
6.Kazi ya Baba/Mlezi---------------------------------------------------------------------------------------------
7. Kazi ya Mama/Mlezi-------------------------------------------------------------------------------------------
8. Je mwanafunzi anacho kilema chochote------------------------------------------------------------
9. Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada au kumtembelea mwanao

| **No.** | **JINA KAMILI** | **KAZI** | **UHUSIANO** | **NAMBA YA SIMU** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**TAREHE---------------------------------------------SAHIHI YA MZAZI/MLEZI-----------------**

***KIAMBATANISHO "B"***

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA SHULE YA SEKONDARI IGUGUNO

*FOMU YA UTHIBITISHO NA KUKUBALI KUJIUNGA*

**A. IJAZWE NA MWANAFUNZI:**

1. Jina kamili la Mwanafunzi ………………………………………………….....
2. Uraia ……………………………………………………………………...
3. Dini ………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa …………………Wilaya………………Mkoa…..……..
5. Shule uliyohitimu kidato cha nne ……………………………………..

**PASSPORT YA MWANAFUNZI**

6. Tahasusi (Combination) ………………………………………………….

Mimi …………………………………………… nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha ………………… naahidi kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Masharti mengine yote ya Shule.

Sahihi ya Mwanafunzi ………………………………… Tarehe ………………………………….

**B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/ MLEZI ATAKAYETAMBULIWA NA SHULE**

1. Jina kamili la Mzazi/ Mlezi ………………………………………….
2. Anuani kamili ……………………………………………………..
3. Kazi unayofanya ……………………………………………………..

**PASSPORT YA MZAZI**

4. Namba ya simu:

a) Nyumbani …………………………………………………… b) Ofisini ……………………………………………………..

c) Mkononi ……………………………………………………..

d) Wilaya ………………………. Mkoa ………………………

Mimi ……………………………….……… Mzazi/ Mlezi wa ……………......……….…

Nimesoma vyema Sheria, Taratibu na Kanuni za Shule, Nakubali/ Sikubali mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari Iguguno naahidi kulipa ada na michango yote kwa wakati na iwapo

**C. UTHIBITISHO WA SERIKALI ZA MITAA**

Jina la M/Kiti wa Mtaa au M/Mtendaji wa Kijiji …………………………………………….

Sahihi …………………………………………….

Simu ……………………………………………...

Muhuri ……………………………………………

***KIAMBATANISHO C***

THE UNITED REPUBLICOF TANZANIA
PRIME MINISTER’S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATION

(To be completed by Government Medical Officer and returned to the Head of school of **Iguguno secondary schoo**l P.O.BOX 55, SINGIDA) To the Medical Officer

…………………………………………
…….

…………………………………………
…….

…………………………………………
……

**RE:**
……………………………………………………….

Please, examine the student mentioned above and comment in his/her health by responding to the following items. Kindly put a Tick (√) or Cross (x) in front of either YES or NO as you find appropriate.

Does a student have problems in connection with?

1. Sight? (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
2. Hearing? (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
3. Speech? (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
4. T.B (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
5. UPT (Girls only) (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
6. Blood pressure? (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
7. Any physical disability? (a) YES ( ) (b) NO ( )
   If yes state………………………………………………………………
   Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this school?
   (a) YES ( ) (b) NO ( )

If no, please state reasons………………………………………………………………………………

Date ……………………………………..Name and signature of M.O…………………………

Designation and stamp…………………………………………